KWILS
KATHERINE WOMEN'S LEGAL SERVICE

(08) 8972 1712
1800 620 108
info@kwils.com.au
www.kwils.com.au

Huduma ya Kisheria ya Wanawake ya Katherine (KWILS) ni huduma ya kisheria ya wanawake kwa wanawake, inayotolewa na wanawake.

KWILS inatambua Mataifa yote katika eneo la Mito Mikubwa kama Wamiliki wa Jadi wa Nchi tunayoishi na kufanya kazi. Tunasherehekea hasa nguvu ya wanawake ambao wamejali watoto wao, familia, na nchi kwa vizazi vingi, na tunaendelea kufanya hivyo.

KWILS hufanya kazi na wanawake **wote**, wa rika **zote**, katika Katherine na eneo la Mito Mikubwa, kufikia wakati ujao ambapo wanawake wote na watoto wao wako salama, wanaoishi kwa utu na heshima.

Huhitaji kuwa na ukaaji wa kudumu au uraia ili kuzungumza na KWILS: tunaweza kukusaidia vyovyote vile na hali yako ya visa.

Wanasheria wetu hutoa ushauri na uwakilishi wa kisheria bila malipo, kwa kuzingatia unyanyasaji wa nyumbani, familia na kijinsia, ulinzi wa mtoto na sheria ya familia (kutengana, talaka, na mipango ya uzazi).

Tunaweza pia kusaidia katika matatizo ya sheria za kiraia kama vile ubaguzi; malalamiko kuhusu polisi, watoa huduma za afya, elimu na Masahihisho; wahasiriwa wa fidia ya uhalifu; matatizo ya nyumba na Centrelink, na sheria ya ajira.

KWILS huajiri Wafanyakazi wa Usaidizi wanaofanya kazi kwa karibu na wateja. Wanaweza kuwa nawe katika miadi au mahakamani, na wanaweza kufanya kazi nawe kufanya kazi hizo zote muhimu zisizo za kisheria kama vile kujaza fomu na maombi, kufanya na kuweka miadi, na marejeleo kwa huduma zingine.

Unapozungumza na wakili, unawaambia hadithi yako, na kile ungependa kitokee. Wakili kisha atakuambia kuhusu chaguzi gani za kisheria ulizonazo. Ni **chaguo lako** nini kuhusu kitu utakachofanya baada ya hapo. Wakili hawezi kukuanzishia kazi yoyote isipokuwa umemwambia afanye.

Ofisi yetu ni ya faragha, na yenye nafasi salama. Wanasheria wetu na wafanyakazi wa usaidizi ni wanawake pia, na wanataka ujisikie salama na kustarehe kila wakati.

Ukipenda, tunafurahi kukutana nawe kwa njia ya simu ya Video, au kuja kwako ambapo unapojisikia salama na kustarehe.

Unaweza kuzungumza na KWILS na mkalimani, ili uweze kutueleza hadithi yako kwa lugha ambayo unajisikia vizuri nayo.

Ikiwa KWILS sio huduma sahihi ya kukusaidia, tutakusaidia kukupatia huduma sahihi. Usiogope kamwe kuomba msaada: ndiyo sababu tuko hapa.

Katika KWILS, tunasikiliza na kuheshimu kwa kina tathmini ya wateja wetu kuhusu usalama wao, na usalama wa familia zao.

Wanasheria wanaruhusiwa kuweka karibu taarifa zote ambazo wateja huwaambia kuwa ni siri. Hata hivyo, lakini kama watu wazima wote katika NT, wafanyakazi wa KWILS wanapaswa kuripoti unyanyasaji wa nyumbani kwa polisi, au ripoti ya lazima kwa Familia za Wilaya ikiwa mtoto ameumizwa au yuko katika hatari ya kudhuriwa.

Popote inapowezekana, KWILS itazungumza nawe kabla ya kutoa ripoti. Pia tutazingatia usalama wa kila mtu, na jinsi gani na lini ni wakati mzuri wa kutoa ripoti.

Ikiwa ungependa kujua zaidi kuhusu sheria za lazima za kuripoti katika NT, unaweza kututumia barua pepe info@kwils.com.au au tupigie kwa 8972 1712.

Kuna habari nyingi zaidi kuhusu KWILS kwenye tovuti yetu - habari kuhusu sheria, jinsi unavyoweza kufanya kazi na KWILS, kujiunga kama mwanachama, na kazi yetu ya kurekebisha sheria na utetezi.

phn NORTHERN TERRITORY An Australian Government Initiative | RURAL Workforce AGENCY NT

*Development and printing of this factsheet has been made been possible by funding from Northern Territory Primary Health Network (NT PHN)*

*This document was translated by The Interpreting & Translating Service NT (ITSNT)*